TANGAZO LA SERIKALI NA. 183 la tarehe 6/3/2020

# SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA 288)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)*

## SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI, 2020

### SEHEMU YA KWANZA

Jina

1. Sheria Ndogo hii itaitwa Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni za Mwaka, 2020.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo-

"Ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma ya uzoaji taka na huduma za usafi;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Chukizo" au "Kero" maana yake ni kitu chochote ambacho kimejengwa au kuwekwa katika hali ya uchafu na kinaweza kusababisha madhara kwa maisha ya binadamu, adha, mazalia ya wadudu na wanyama hatari au madhara kwenye chakula na vyanzo vya maji;

"dampo" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kama eneo maalum mbali na makazi ya watu kwa ajili ya kutupa taka taka za aina yoyote;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa Kinondoni;

"Huduma" maana yake ni pamoja na usafishaji, ukusanyaji, uondoshaji na usafirishaji wa taka;

"Kaya" maana yake ni baba mama na watoto na ni pamoja na mtu anayeishi peke yake kwa kujitegemea, watu waishio pamoja, mpangaji katika nyumba ya makazi au biashara;

"lundo la taka" maana yake ni pamoja na vifaa na zana chakavu, mabaki ya samani ambayo haihusishi mabaki ya vifaa vya ujenzi au wanyama waliokufa;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mmiliki" maana yake ni mmiliki wa nyumba ya makazi au biashara, taasisi, ofisi, nyumba ya biashara, mpangaji,

wakala au mtu yeyote mwenye dhamana ya kuishi katika nyumba;

"nyumba ya makazi" maana yake ni jengo lolote linalotumiwa kwa kuishi, na inajumuisha pia ardhi inayozunguka nyumba husika.

"taka hatari" maana yake ni taka kama ilivyotafsiriwa chini ya kifungu cha 133 (5) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"taka ngumu" maana yake ni aina zote za taka zinazozalishwa majumbani, kwenye taasisi, maeneo ya biashara na viwandani lakini hazihusishi maji taka au taka za kimiminika;

Sura ya 191

"taka za majengo ya biashara" maana yake ni taka zote zinazozalishwa kutoka katika majengo ya biashara na viwanda pamoja na taka zitokanazo na utoaji wa huduma mbalimbali lakini hazihusishi taka zinazozalishwa majumbani;

"Ukaguzi wa kiafya" maana yake ni ukaguzi utakaofanywa na Halmashauri au Afisa Mwidhiniwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hizi;

"Wakala" maana yake ni Kampuni, Taasisi, Kikundi jamii (CBO) au mtu yeyote aliyeteuliwa na Halmashuri kwa ajili ya kutoa huduma ya kuzoa taka katika eneo au sehemu ya eneo la Halmashauri.

## SEHEMU YA PILI
### USAFI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

4. Kila mkazi au mfanyabiashara anayemiliki nyumba au eneo la biashara atahakikisha kwamba anafanya usafi wa mazingira kuzunguka makazi au eneo lake kwa kuhakikisha kwamba-

(a) majani yanayozunguka nyumba yake au eneo lake yanalimwa,yanakatwa katika eneo kuanzia mwanzo wa mipaka ya barabara ya mbele ya nyumba yake au eneo lake lote;

(b) takataka ngumu zote ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki zitakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;

(c) takataka laini zote ambazo zinaweza kuoza zitachimbiwa shimo la taka na kutupwa humo; na

(d) nyumba au kiwanja au eneo lolote ambalo halijaendelezwa kuhakikisha linafanyiwa usafi katika eneo hilo mara kwa mara.

Usafi wa mifereji ya maji ya mvua.

5. Mmiliki wa nyumba ataondoa uchafu kama vile mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mfereji wa maji ya mvua unaozunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mfereji huo unakuwa msafi na imara siku zote.

Uwekaji taa za nje ya nyumba

6. Mmiliki wa nyumba, mpangaji au mfanyabiashara ataweka taa zenye mwanga nje ya jengo analoishi au analolitumia kwa shughuli yoyote na atatakiwa kuiwasha wakati wa usiku.

Kupaka rangi majengo

7. Mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara atahakikisha kwamba anapaka rangi nyumba yake au majengo yote anayoyatumia kila itakapochakaa.

Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia ya mbu.

8. Mmiliki wa jengo au mtumiaji wa jengo atahakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.

Biashara ya miwa na matunda

9. Mfanyabiashara ya matunda, mboga mboga au miwa, au bidhaa yeyote atahakikisha kuwa ana chombo maalumu cha kuhifadhia maganda au mabaki ya matunda.

Kupuliza dawa

10. Mtu yeyote haruhusiwi kuendesha biashara ya kupuliza dawa au biashara ya kuuwa wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila kuwa na kibali kinachotambuliwa na Serikali na awe na leseni hai kutoka Halmashauri.

Matengenezo ya magari, pikipiki, mitambo na kuegesha magari mabovu

11.-(1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

(2) Mtu yeyote haruhusiwi kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo.

(3) Mtu yeyote haruhusiwi kuegesha magari mabovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi au barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo.

## SEHEMU YA TATU
### UIMARISHAJI WA AFYA

Usalama wa maji ya kunywa.

12. Mkazi yeyote atahakikisha kwamba maji yote yanayotumika kunywa ni safi na salama kwa kuyachemsha bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji.

Kutengeneza na kuuza vyakula.

13. Mtu yeyote haruhusiwi kutengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za afya na amepata kibali kutoka kwa Halmashauri au kwa Afisa Mwidhiniwa.

Uuzaji vyakula vilivyopikwa.

14. Mtu yeyote anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa atahakikisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi na kuwekwa kioo kuzuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.

Usalama wa vyakula.

15. Mtu yeyote haruhusiwi kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini, vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza.

Uzuiaji wa shughuli mbalimbali wakati wa magonjwa ya mlipuko

16. Afisa Mwidhiniwa anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

Ukamataji wa vyombo vilivyotumika kuhifadhia chakula

17.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata vyakula, vyombo au vifaa vingine vyovyote vitakavyokuwa vinatumika mara baada ya kutolewa amri ya zuio la kutofanyika kwa shughuli ya uuzaji wa vyakula wakati wa magonjwa ya mlipuko.

(2) Endapo vyakula vitakavyokamatwa vitakuwa ni vile ambavyo vinaharibika kwa haraka Halmashauri itaharibu vyakula hivyo.

(3) Endapo vyakula vitakavyokamatwa vitakuwa haviharibiki kwa haraka Halmashauri itakuwa na jukumu la kuvihifadhi hadi mwisho wa amri ya zuio na Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa Halmashauri au Afisa wa Halmashauri.

Maduka ya nyama

18.-(1) Mmiliki yeyote wa duka la kuuzia nyama atahakikisha kwamba duka lake-

(a) ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa marumaru nyeupe hadi urefu wa mita 6 kutoka usawa wa sakafu;

(b) lina maji safi, na misumeno ya kukatia nyama;

(c) lina milango ya vioo na jokofu la kuhifadhia nyama

na sehemu za mizani; na

(d) lina pipa la kuhifadhia taka taka.

(2) Muuzaji yeyote wa nyama atatakiwa kuvaa vazi jeupe pamoja na aproni nyeupe,viatu vya kufunika na sharti awe anapimwa afya kila baada ya miezi sita.

Kuchinja na kuuza nyama mahali pasiporuhusiwa

19. Mtu yeyote haruhusiwi kuchinja au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyokuwa machinjio au maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.

Uendeshaji wa biashara ya Nyumba za kulala wageni na Hosteli

20.-(1) Mmiliki wa nyumba za kulala wageni, hosteli au nyumba za biashara atahakikisha anapata kibali kutoka Halmashauri kabla ya kuanza biashara.

(2) Endapo mmiliki hajakidhi masharti ya kiafya Halmashauri inaweza kuzuia kibali cha kuendesha biashara ya nyumba za kulala wageni, hosteli, au nyumba za biashara mpaka hapo mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti yaliyotolewa na Halmashauri.

Mahitaji ya nyumba za wageni, migahawa na hosteli

21. Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, mgahawa na hosteli kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa katika majengo hayo kuna-

(a) mwanga na hewa ya kutosha;
(b) nafasi na vifaa (samani ) za kutosha;
(c) mfumo wa uondoshaji wa maji taka na taka ngumu wa kuaminika;
(d) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;
(e) vyoo na mabafu kwa jinsia zote na watu wenye ulemavu;
(f) vifaa vya zima moto;
(g) tanki la kuhifadhia maji safi; na
(h) vyoo na bafu vilivyosakafiwa kwa marumaru na kuta zake zimewekwa marumaru kiasi cha mita sita kutoka usawa wa sakafu.

Upimaji wa afya

22.-(1) Mmiliki wa hoteli, mgahawa, baa, duka la nyama, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni na duka la pombe atahakikisha kuwa wafanyakazi wake wote

wamepimwa afya kila baada ya miezi sita na watalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha shilingi elfu tano (Tsh.5,000/=).

(2) Mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza atalazimika kupimwa afya kila baada ya miezi sita na atalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha shilingi elfu tano (Tsh.5,000/=).

(3) Mmiliki yeyote atakayeruhusu mtoa huduma yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya yake kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), atakuwa ametenda kosa.

Uwezo wa kukagua

23. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wowote kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Kufungwa kwa jengo la biashara lisilokidhi masharti ya afya

24. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii.

Ada ya ukaguzi wa afya

25. Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya ambayo italipwa kwa mwaka kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara ambayo viwango vyake vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Muda wa kulipa ada

26.-(1) Ada ya ukaguzi wa afya italipwa kila mwanzo wa mwaka wa fedha wa Halmashauri yaani mwezi Julai.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ada katika kipindi cha miezi miwili baada ya mwaka wa fedha kuanza atawajibika kulipa kiwango hicho pamoja na adhabu ya asilimia hamsini ya kiwango atakachokuwa anadaiwa.

## SEHEMU YA NNE
## UZOAJI TAKA

Ada ya uzoaji taka

27.-(1) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kutoka kwa kila kaya au jengo la biashara kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(2) Ada ya kila mwezi italipwa kila mwisho wa mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo atakayolipwa na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.

(3) Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Uanzishwaji wa Vikundi Jamii (CBOs)

28. Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa Vikundi Jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Wajibu wa kuwa na pipa la taka

29. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha kuwa ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili ya kuhifadhia taka ngumu kabla hazijachukuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kwenda kutupwa.

Kutupa taka katika sehemu maalum

30. Mkazi yeyote atahakikisha kwamba anatupa uchafu au taka katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalum yaliyotengwa.

Marufuku kutupa taka hovyo

31. Mtu yeyote haruhusiwi kutupa taka, uchafu wowote au kuacha kuwepo takataka mahali popote ambapo hapajatengwa kwa shughuli hiyo.

Uhifadhi maji taka

32. Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.

Kutiririsha maji taka

33. Mtu yeyote haruhusiwi kutiririsha au kuelekeza maji

kutoka vyooni, bafuni, karoni, baada ya kufua au kuosha vyombo kwenda sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka.

Taka za viwanda

34.-(1) Kiwanda chochote hakiruhusiwi kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya na kusababisha kero kwa wakazi wa eneo la Halmashauri.

(2) Mmiliki wa kiwanda atahakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na takataka nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe hai wengine.

Uteuzi wa Wakala

35. Halmashauri inaweza kuteua Kampuni, kikundi, kikundi cha jamii au mtu binafsi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

## SEHEMU YA TANO
## UJENZI NA MATUMIZI YA VYOO

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

36. Mmiliki wa nyumba au mpangaji atahakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi, imara na madhubuti kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote.

Umbali wa kujenga choo

37. Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa zaidi ya mita sitini (60) kutoka chanzo chochote cha maji.

Vyoo vya umma

38.-(1) Halmashauri inaweza kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo.

(2) Mtu binafsi, kikundi au taasisi ambaye amejenga choo cha umma katika eneo lake binafsi atalipia ushuru wa kuendesha biashara hiyo kulingana na mwongozo au makubaliano au mkataba kati yake na Halmashauri.

(3) Vyoo hivyo vitamilikiwa na Halmashauri au kwa ubia na wajenzi na vitakuwa ni vya kulipia kama itakavyokuwa imeelekezwa na Halmashauri katika mkataba wake na

mawakala watakaopewa kusimamia vyoo hivyo.

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

39. Mtu, kikundi au taasisi yenye lengo la kukutanisha watu kwa madhumuni ya ujenzi, sherehe au sehemu yoyote ambayo itakutanisha watu kwa muda maalum na endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu, atatakiwa kujenga vyoo kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri.

Vyoo katika majengo ya biashara

40. Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo viwili au vitatu vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hii kwa ajili ya matumizi ya wateja wake wa jinsia zote pamoja na watu wenye ulemavu.

Ilani ya kujenga choo

41. Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo, choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani ya siku thelathini (30) kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

Kufungwa kwa jengo

42. Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 41 Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara hadi hapo hali hiyo itakaporekebishwa.

Ilani ya kuondoa kero

43.- (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ya siku saba (7) kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

Halmashauri kuteua mkaguzi

44. Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote kuwa mkaguzi kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa usafi

katika eneo la Halmashauri.

Mamlaka ya kutoa adhabu ya papo kwa papo

45. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hii, Mkaguzi atakuwa na mamlaka ya kutoa adhabu ya papo kwa papo kwa mtu yeyote atakayekutwa amechafua mazingira kwa kutupa takataka mahali popote pasiporuhusiwa ilimradi kuwa adhabu hiyo izingatie masharti ya Sheria Ndogo hii.

Makosa

46. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atamzuia au kujaribu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii;

(c) atamwaga takataka barabarani, kwenye mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni, au mahali popote hadharani au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;

(d) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;

(e) atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;

(f) ataosha magari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;

(g) atafanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, kuendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za

mipango miji;

(h) ataanzisha au kufungua karakana katika majengo au majumba au maeneo ya makazi;

(i) ataenda haja ndogo au kubwa hovyo barabarani, uchochoroni, upenuni au mahali popote ambapo siyo chooni; au

(j) atashindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo.

Adhabu

47. Mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/-) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Tangazo la Serikali namba 202 la mwaka, 2002

48. Sheria Ndogo hii inafuta Sheria ndogo ya (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni za Mwaka, 2002.

Tangazo la Serikali namba 353 la mwaka, 2001

49. Sheria Ndogo hii inafuta Sheria Ndogo ya Sheria Ndogo ya Ada ya Usimamizi na Uchukuaji Taka ya Halmashauri ya Manispaa Kinondoni ya Mwaka 2000 (The Kinondoni Municipal Council (Waste Management and Refuse Collection Fees By-Laws) pamoja na marekebisho yake yote za Mwaka, 2000.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 25)*

Ada ya Ukaguzi wa Afya

| Na. | Aina ya biashara | Ada kwa mwaka Tsh. |
|---|---|---|
| 1. | Maduka ya pombe ya jumla na rejareja | 5,000/= |
| 2. | Migahawa na Mama Lishe | 2,500/= |
| 3. | Nyumba za wageni (Guest House) na Hoteli | 10,000/= |
| 4. | Kumbi za starehe au mikutano | 10,000/= |
| 5. | Majengo mengine ya biashara | 5,000/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 27(1))*

Ada ya Uzoaji Taka

| Na | Aina ya jengo | Kiwango kwa Tshs |
|---|---|---|
| 1 | (a) Eneo la makazi (kaya) (kwa mwezi)<br>(b) Mabalozi (kila ubalozi) (kwa mwezi) | (a) 3,000-30,000<br>(b) 500,000/= |
| 2 | Mahali panapouzwa barafu ( kwa mwezi) | 50,000/= |
| 3 | Mgahawa (kwa mwezi) | 5000-30,000/= |
| 4 | Nyumba ya wageni ( kwa mwezi) | 30,000/= |
| 5 | Zahanati (kwa mwezi) | 20,000/= |
| 6 | Kituo cha afya (kwa mwezi) | 50,000/= |
| 7 | Maabara | 30,000-50,000/= |
| 8 | Kliniki | 30,000-50,000/= |
| 9 | (a) Taka ngumu za Viwandani (taka zisizohatarishi) (kwa tripu/safari moja)<br>(b) Taka hatarishi za viwandani (kwa kila tani) | (a) 500,000/=<br>(b) 200,000/= |
| 10 | Hospitali ( kwa mwezi) | 300,000/= |
| 11 | Maduka ya jumla ( kila mwezi) | 30,000/= |
| 12 | Maduka ya rejareja ( chakula na bidhaa nyingine) (kila mwezi) | 10,000-20,000/= |
| 13 | Shule ya binafsi ya kutwa (kila mwezi)<br>Shule ya binafsi ya bweni (kila mwezi) | 25,000/=<br>30,000/=<br>40,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 183 (linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| | Taasisi (kwa mwezi) | |
| 14 | Kituo cha kutwa cha kutunzia watoto ( kila mwezi) | 14,000/= |
| 15 | Duka la jumla vyakula (kila mwezi) | 20,000/= |
| 16 | Duka la pombe (kila mwezi) | 50,000/= |
| 17 | Butcher (kila mwezi) | 20,000/= |
| 18 | Duka la dawa (kila mwezi) | 20,000/= |
| 19 | Soko ( kwa safari) | 250,000/= |
| 20 | Magenge ( kila mwezi) | 5,000-20,000/= |
| 21 | Mama lishe/ baba lishe ( kwa siku) | 5,000/= |
| 22 | Daladala – ushuru kwa mwezi | 30,000/= |
| 23 | Biashara ndogo ndogo. Sekta isiyo rasmi (kwa mwezi) | 2,000/= |
| 24 | Dobi kwa siku | 2,000/= |
| 25 | Fundi seremala (kwa mwezi) | 5,000- 60,000/= |
| 26 | Fundi viatu ( kwa mwezi) | 2,000-10,000/= |
| 27 | Supermarket ( kwa mwezi) | 250,000/= |
| 28 | Meza ndani ya soko – kwa mwezi | 4,000/= |
| 29 | Ada ya kutupa taka kizimbani – kwa mwezi | 4,000/= |
| 30 | Ada ya kutupa taka kutoka kwenye mkokoteni ndani ya kizimba – kwa mwezi | 4,000/= |
| 31 | Ukarabati wa vifaa vya umeme kama televisheni | 6,000/= |
| 32 | Fundi cherehani aliesajiliwa (kila mwezi) | 5,000-20,000/= |
| 33 | Saluni iliyosajiliwa (kila mwezi) | 5,000-20,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 34 | Kituo cha Petrol (kila mwezi) | 250,000/= |
| 35 | Kituo cha mafuta ya taa (kila mwezi) | 10,000/= |
| 36 | Stoo ya Mkaa (kila safari) | 20,000-250,000/= |
| 37 | Ghala ( kila mwezi) | 50,000/= |
| 38 | Hoteli (kila mwezi) | 250,000/= |
| 39 | Nyumba ya wageni ( kila mwezi) | 40,000/= |
| 40 | Ada ya magari ya kubebea taka (kwa mwaka) | 250,000/= |
| 41 | Magari ya maji taka (kwa mwaka) | 250,000/= |
| 42 | Kijiko – wheel loader (kwa masaa 8) | 600,000/= |
| 43 | Kuzoa taka kwa trip moja | 250,000/= |
| 44 | Magari makubwa ya kushusha na kupakia abiria ndani ya soko | 20,000/= |
| 45. | Ofisi<br>Wafanyakazi 01-10 (kila mwezi)<br>Wafanyakazi 11-20 (kila mwezi)<br>Wafanyakazi 21-30 (kila mwezi)<br>Wafanyakazi 31-50 (kila mwezi)<br>Wafanyakazi 51-100 (kila mwezi)<br>Wafanyakazi 101 na kuendelea (kila mwezi) | <br>20,000/=<br>40,000/=<br>50,000/=<br>70,000/=<br>100,000/=<br>200,000/= |
| 46. | Karakana (kila mwezi) | 20,000/= |
| 47. | Bar (kwa kila mwezi) | 250,000/= |
| 48. | Biashara ya mbao (kwa kila mwezi) | 250,000/= |
| 49. | Biashara ya kufyatua na kuuza tofali (kwa kila mwezi) | 5,000-50,000/= |
| 50. | Hardware (kwa kila mwezi) | 250,000/= |
| 51. | Biashara za matunda (kwa kila siku) | 5,000-50,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 52. | Biashara ya mchanga, kokoto na kifusi | 5,000-50,000/= |

__________

JEDWALI LA TATU

__________

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 41)*

__________

ILANI YA KUJENGA CHOO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha (41) cha Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ya mwaka, 2020.

SEHEMU 'A'

Ndugu…………………..............wa Mtaa/……………Kata ya…………………

Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe……mwezi………..mwaka….

Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma*/ Namba………… iliyopo eneo la ………………katika Kitongoji/Mtaa*……….Kijiji cha……………Kata ya………….

Imekuwa haina choo/ choo kimejaa/kimeharibika* hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo;

(1) ………………………………………………………………………………

(2) ………………………………………………………………………………

(3) ………………………………………………………………………………

(4) ………………………………………………………………………………

SEHEMU 'B'

Unapewa muda wa siku thelathini (30) tu tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza maelekezo yote yaliyoelezwa katika sehemu 'A' ya Ilani hii,

SEHEMU 'C'

Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe……………….endepo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itakuchukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

………………………………..

AFISA MWIDHINIWA

| IMETOLEWA NA; | IMEPOKELEWA NA; |
|---|---|
| Jina;……………………………….…. | Jina;…………………………………. |
| Saini………………………………… | saini……………………………….... |
| Wadhifa……………………...……... | wadhifa…………………………….. |
| Tarehe……………………….…….. | Tarehe…………………………….... |

*Futa lisilotakiwa.

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 43(1))*

ILANI YA KUONDOA KERO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha (43)(1) cha Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ya mwaka 2020.

SEHEMU 'A'
Ndugu…………………..............wa Mtaa/ ……………Kata ya…………………
Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe……mwezi………..mwaka….
Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma/kiwanja* iliyopo eneo la……………………………………………………………………….kumekutwa machukizo/kero/uchafu*; kama ifuatavyo;

1) ……………………………………………………………………
2) ……………………………………………………………………
3) ……………………………………………………………………
4) ……………………………………………………………………

SEHEMU 'B'
Kwa ilani hii unaamriwa kurekebisha/kuondoa/kusafisha* kwa;

1. ……………………………………………………………………
2. ……………………………………………………………………
3. ……………………………………………………………………
4. ……………………………………………………………………

SEHEMU 'C'
Unapewa muda wa siku saba (7) tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza yote yaliyoelezwa katika sehemu 'B' ya Ilani hii, kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kulazimika kukupa taarifa nyingine.

…………………………………..
AFISA MWIDHINIWA

| IMETOLEWA NA; | IMEPOKELEWA NA; |
| --- | --- |
| Jina;………………………. | Jina;…………………………………. |
| Saini……………………… | saini……………………………….... |
| Wadhifa…………………... | wadhifa…………………………….. |
| Tarehe…………………….. | Tarehe…………………………….. |

*Futa lisilohusika

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imebandikwa kwenye Sheria ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa katika kikao cha baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kilichofanyika tarehe 20 Desemba, 2018 na kushuhudiwa.

Lakiri hiyo ilibandikwa mbele ya:-

……………………..…………..
ARON T. KAGURUMJULI,
*Mkurugenzi wa Halmashauri Halmashauri ya Kinondoni*

L.S

……………………..…………..
BENJAMINI K. SITTA,
*Mstahiki Meya wa Halmashauri Halmashauri ya Kinondoni*

NAKUBALI,

Dodoma
8 Februari, 2020

…….……..……………
SELEMANI SAID JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*